Swahili | Kiswahili

# Kujiandikisha katika shule ya msingi kwa 2026

Kuanza shule ni wakati wa kusisimua kwa watoto, wazazi pamoja na walezi. Sisi tunataka kukusaidia kufanya mchakato wa kujiandikisha kuwa rahisi iwezekanavyo kwako.



Katika Victoria, mtoto wako ana haki ya kuhudhuria shule ya ujirani aliyotengewa ('shule yako ya mtaani') chini ya *Sheria ya Marekebisho ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2006*.

Unaweza pia kutuma maombi ya nafasi katika shule ambayo si shule ya karibu nawe. Shule itazingatia ombi lako kulingana na Sera ya Uwekaji Wanafunzi. Kwa habari zaidi juu ya Sera ya Uwekaji Wanafunzi, tembelea ukurasa wa Kujiandikisha katika shule.

## Ratiba mpya ya jimbo zima kwa Maandalizi (Prep)

Mwaka wa kwanza wa shule ya msingi unaitwa Maandalizi au Prep. Tumetoa ratiba ya uandikishaji ya Maandalizi kwa shule zote za msingi za serikali ya Victoria za kufuata (tazama ukurasa wa 4). Ratiba ya matukio inalenga kukusaidia kuelewa ni lini na jinsi ya kumsajili mtoto wako katika Maandalizi kwa mwaka wa shule wa 2026.

## Je, ni lini ninapaswa kumwandikisha mtoto wangu katika mwaka wake wa kwanza wa shule ya msingi?

Mtoto wako lazima awe na umri wa miaka 5 ifikapo tarehe 30 Aprili katika mwaka ambao anaanza shule.

Kusoma shuleni ni lazima kwa watoto ambao wamefikisha miaka 6.

Ili kumwandikisha mtoto wako katika shule ya msingi ya serikali ya Victoria kwa mwaka wa shule wa 2026, tuma maombi ya kujiandikisha kwenye shule kabla ya tarehe 25 Julai 2025.

## Je, ninawezaje kumwandikisha mtoto wangu katika mwaka wa kwanza wa shule ya msingi?

Chukua hatua hizi ili kumwandikisha mtoto wako katika mwaka wa kwanza wa shule ya msingi:

1. Tafuta shule yako ya karibu kwenye tovuti ya Tafuta Shule yangu (tazama hapa chini).
2. Wasiliana na shule ya msingi ya serikali ili uombe kufanya ziara ya shule au upate maelezo zaidi kuhusu shule na mchakato wa kutuma maombi ya kujiandikisha.
3. Pakua kifurushi cha taarifa za uandikishaji cha Maandalizi (Prep) kutoka Kujiandikisha katika Maandalizi (Prep). Kifurushi kitapatikana kuanzia Jumanne tarehe 22 Aprili 2025 na kitajumuisha fomu ya maombi. Shule inaweza pia kukupa nakala ya fomu ili ujaze.
4. Tuma maombi ya kujiandikisha kwa shule ya Maandalizi **kufikia kabla ya Ijumaa tarehe 25 Julai 2025**.
5. Utaarifiwa kuhusu matokeo ya ombi lako **kati ya Jumatatu tarehe 28 Julai na Ijumaa tarehe 8 Agosti 2025**. Kama ukipokea ofa, unapaswa kukubali ofa **kufikia kabla ya Ijumaa tarehe 22 Agosti 2025**.
6. Shiriki katika maelezo ya uandikishaji na vipindi vya mpito **katika Muhula wa 4 2025**.
7. Mtoto wako ataanza Maandalizi **kutoka Jumatano tarehe 28 Januari 2026**.

## Je, nitapataje shule yangu ya karibu?

Tafuta shule yako ya karibu kwenye tovuti ya Tafuta Shule yangu kwa kufuata hatua zilizo hapa chini:

1. Ingiza findmyschool.vic.gov.au kwenye kivinjari chako.
2. Weka anwani yako ya makazi ya kudumu chini ya 'Enter your address to get started'.
3. Chagua 2026 chini ya 'Enrolment year'. **Kumbuka:** Maeneo ya shule ya 2026 yatapatikana mwishoni mwa Muhula wa 1, 2025.
4. Chagua Msingi chini ya 'School type'.

Kisha ramani itaonyesha anwani yako, shule ya karibu nawe, na kwenye upande wa kushoto maelezo ya mawasiliano ya shule. Ukisogeza chini, itakuonyesha pia shule tano zilizo karibu zaidi na anwani yako.

Wewe unaweza pia kutafuta kwa jina la shule chini ya 'Search for school'.

## Je, mtoto wangu anaweza kutia ombi la shule ya msingi ya serikali ambayo sio shule yetu ya mtaa?

Ndiyo, wewe unaweza kutia ombi kwa shule nyingine mbali na shule ya eneo lako. Shule itazingatia ombi lako kulingana na Sera ya Uwekaji Wanafunzi na nafasi inayopatikana. Unaweza kupata taarifa juu ya jinsi maombi yanapewa kipaumbele kwenye ukurasa wa Kujiandikisha katika shuleni.

## Nini hutokea ikiwa nitapokea barua inayosema kwamba ombi langu la kujiandikisha halikufaulu?

Wewe unapaswa kutia ombi la kumwandikisha mtoto wako katika shule nyingine. Mtoto wako amehakikishiwa nafasi katika shule yake ya karibu. Shule ya mtaani ya mtoto wako huchaguliwa kwa kuangalia anwani yake ya kudumu ya makazi. Tembelea Tafuta Shule yangu ili kutafuta shule ya mtaani ya mtoto wako. Ukurasa wa Kujiandikisha shuleni unaweza pia kukusaidia wewe ili kuthibitisha anwani ya mtoto wako kwa ajili ya kujiandikisha.

Wewe unaweza pia kukata rufaa kwa uamuzi huo. Ukurasa wa Kujiandikisha katika Maandalizi (Prep) una maelezo kuhusu mchakato wa kukata rufaa ya matokeo ya ombi la kujiandikisha.

## Je, nini hutokea ikiwa nitakosa muda wa kujiandikisha?

Unaweza kutuma maombi ya kumwandikisha mtoto wako katika Maandalizi kwa mwaka wa shule wa 2026 wakati wowote kuanzia Muhula wa 2, 2025.

Ingawa umeombwa kuwasilisha ombi la kujiandikisha kabla ya Ijumaa, tarehe 25 Julai 2025, maombi yanayotufikia baada ya tarehe hii bado yatakubaliwa kutoka kwa familia ambazo zimekosa ratiba ya matukio ya kujiandikisha, zimehama makazi ya kudumu au zimewasili hivi karibuni Victoria.

Maombi ya kujiandikisha yatakayowasilishwa baada ya tarehe 25 Julai 2025 yatashughulikiwa na shule kadri yanavyopokelewa, kwa mujibu wa Sera ya Uwekaji Wanafunzi wa idara.

## Je, ninaweza kupata wapi maelezo zaidi kuhusu kujiandikisha katika shule ya msingi?

Wewe unaweza kuuliza shule ya msingi ya mtaa wako kwa maelezo zaidi kuhusu mchakato wa uandikishaji wa Shule ya Maandalizi.

Mwanzoni mwa Muhula wa 2, 2025 wewe unaweza pia kupata kijifurushi cha maelezo kuhusu mchakato wa uandikishaji wa Maandalizi kwenye ukurasa wa Kujiandikisha katika Maandalizi (Prep).

Ikiwa wewe unahitaji usaidizi wa kutafsiri kijifurushi cha maelezo, tafadhali zungumza na shule ya msingi ya eneo lako kwa usaidizi.

## Je, nitawasiliana na nani kwa usaidizi?

Mratibu wa Mpito, Afisa wa Uandikishaji au Mkuu wa shule ya msingi unayotaka kutia ombi anaweza kukusaidia kwa maswali yoyote ambayo unaweza kuwa nayo kuhusu mchakato wa kujiandikisha.

## Viungo muhimu

Tafadhali tafuta viunganishi muhimu hapa chini ambavyo vinaweza kukusaidia wakati mtoto wako anapoanza shule ya msingi:

Tafuta Shule yangu – findmyschool.vic.gov.au

Taarifa kuhusu maeneo ya shule – vic.gov.au/school-zones

Kujiandikisha katika Maandalizi (Prep) – vic.gov.au/enrolling-foundation-prep

Kujiandikisha shuleni – vic.gov.au/how-choose-school-and-enrol

Ulemavu pamoja na elimu jumuishi – vic.gov.au/disability-and-inclusive-education

Mawasiliano ya ofisi ya mkoani – vic.gov.au/office-locations-department-education

# Rekodi ya matukio ya 2025-26

| Tarehe za 2025 | Shughuli |
|---|---|
| **Muhula wa 2: Jumanne 22 Aprili 2025 - Ijumaa 4 Julai 2025** | |
| **Mihula ya 1 na 2, 2025** | Shule za msingi hufanya ziara, vipindi vya maelezo pamoja na shughuli zinginezo kwa familia zinazotafuta uandikishaji wa Shule ya Maandalizi (Prep) kwa ajili ya watoto wao kwa 2026. |
| **Kabla ya mwanzo wa Muhula wa 2, 2025** | Maeneo ya shule kwa mwaka wa shule wa 2026 yataonekana kwenye findmyschool.vic.gov.au<br>Wazazi na walezi wanapaswa waende kwenye findmyschool.vic.gov.au ili kupata shule yao ya ujirani iliyoteuliwa (shule ya mtaa) kwa 2026.<br>Kijifurushi cha Maelezo ya Kujiandikisha kwa Wazazi na Walezi kinapatikana kwa kupakuliwa kutoka Kujiandikisha katika Maandalizi (Prep). |
| **Kuanzia Wiki ya 1, Muhula wa 2 2025** | Shule za msingi zinaweza kusambaza Vifurushi vya Maelezo ya Uandikishaji kwa familia zinazotarajiwa pamoja na jumuiya yao. |
| **Kuanzia Wiki ya 1, Muhula wa 2 2025** | **Maombi ya kujiandikisha hufunguliwa** –wazazi na walezi wanaweza kuwasilisha ombi lao la kujiandikisha lililokamilika kwa shule ya msingi ya serikali kuanzia tarehe hii. |
| **Muhula wa 3: Jumatatu 21 Julai 2025 - Ijumaa 19 Septemba 2025** | |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 25 Julai 2025** | **Maombi ya kujiandikisha yanayodaiwa** –wazazi na walezi huwasilisha maombi yao ya kujiandikisha yaliyokamilika kwa shule ya msingi ya serikali kabla ya tarehe hii. |
| **Kati ya Jumatatu 28 Julai na Ijumaa 8 Agosti 2025** | Shule za msingi huwaarifu wazazi na walezi kwa maandishi kuhusu matokeo ya uandikishaji wa Maandalizi (Prep), kulingana na Sera ya Uwekaji Wanafunzi ya idara. Hii inaweza kujumuisha barua ya ofa, barua ya kuthibitisha kujiandikisha, au barua ya maombi ambayo haijafanikiwa.<br>Wazazi na walezi waliotuma barua ya maombi ambayo haijafanikiwa wanaweza kuanza kuwasilisha rufaa iya maandishi kwa shule ya msingi. |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 22 Agosti 2025** | Wazazi na walezi waliotumiwa barua ya ofa ya nafasi wataonyesha kukubaliwa kwa nafasi ya mtoto wao kabla ya tarehe hii. |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 22 Agosti 2025** | **Tarehe ya mwisho** kwa wazazi na walezi kuwasilisha rufaa iliyoandikwa kwa shule ya msingi. |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 5 Septemba 2025** | Shule za msingi huwaarifu wazazi na walezi wote, kwa maandishi, kuhusu matokeo ya rufaa yao kufikia tarehe hii. |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 19 Septemba 2025** | **Tarehe ya kufunga** kwa wazazi na walezi kuwasilisha rufaa ya kimaandishi ya kutopanga shule kwa Mkurugenzi wa Mkoa husika, ambapo wameshindwa na rufaa yao kwa shule ya msingi. |
| **Muhula wa 4: Jumatatu tarehe 6 Oktoba 2025 - Ijumaa tarehe 19 Desemba 2025** | |
| **Katika Muhula wa 4, 2025** | Shule za msingi huandaa vipindi vya mpito. |
| **Ifikapo kabla ya Ijumaa tarehe 31 Oktoba 2025** | Mikoa inawaarifu wazazi na walezi wote kwa maandishi kuhusu matokeo ya rufaa za Mkurugenzi wa Mkoa wa kutopangiwa ifikapo tarehe hii. Hii inatumika tu kwa rufaa zilizopokelewa kabla ya tarehe ya kufunga ya Ijumaa 19 Septemba 2025. |